BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

# BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI

## MKUTANO WA PILI

**Kikao cha Tano – Tarehe 17 Februari, 2026.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua Itasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Fedha na Mipango:**

Taarifa ya Muelekeo wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2026/2027.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti:**

Hotuba ya maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Taarifa ya Muelekeo wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2026/2027.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

25. MHESHIMIWA AZZA JANUAR JOSEPH (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

    Tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa hatua iliyochukua ya kukipatia Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) boti maalum kwa ajili ya uokozi pale yanapotokea maafa baharini.

a) Je, boti hizi zina uwezo wa kubeba majeruhi wangapi kwa wakati mmoja.

b) Je, ni eneo gani boti hizo huwekwa ili kuweza kuwahi kwa wakati katika eneo la maafa pale yanapotokea na kuzinusuru roho za majeruhi hao.

130. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kumekuwa na ongezeko kubwa la uingizaji wa kilevi kinachojulikana kama *Double Kick* kwa siku za karibuni hapa Zanzibar, kinyume na Sheria ya Vileo Nam. 9 ya mwaka 2020. Kilevi hiki kina zaidi ya asilimia 43 ya *alcohol*, jambo linalopelekea athari kubwa kwa vijana wetu ambao wanatumia kinywaji hiki.

(a) Kwa kiwango kipi Serikali inalitambua tatizo hili la uingizwaji wa kilevi cha *Double Kick* hapa Zanzibar.

(b) Je, Serikali inawaambia nini wananchi wake hususan vijana juu ya athari ya *Double Kick* kwa mustakbali wa maisha yao.

(c) Je, uingizwaji kiholela wa *Double Kick* pamoja na kuuzwa kwake katika maduka ya kawaida hapa Zanzibar hususan wakati wa usiku, unakubalika vipi kwa mujibu wa Sheria ya Vileo Nam. 9 ya mwaka 2020.

## <u>Wizara ya Fedha na Mipango:</u>

197. MHESHIMIWA KHAMIS MOHAMMED AMRAN (Jimbo la Mkoani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Ninaipongeza Serikali ya Awamu ya Nane kwa kuongeza kasi ya kuleta maendeleo kwa wananchi wa Zanzibar.

Je, ni utaratibu gani unaotumika katika kugawa miradi ya kimkakati katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

79. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Elimu na Mafunzo ya Amali:

    Kwa kuwa Serikali ina mpango wa kujenga skuli ya ghorofa katika eneo la kilimo lililopo katika Mtaa wa Kilimo Machomane, ambalo linamilikiwa na Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo.

    Je, ni lini eneo hili litakabidhiwa kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ili ujenzi wa skuli hiyo uanze rasmi.

187. MHESHIMIWA SEIF HAMAD SULEIMAN (Mwakilishi Jimbo la Ole)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

    Kwa kuwa Zanzibar imefanikiwa kuwa na vyuo vingi vya elimu ya kati ambavyo vimeanzishwa na wazawa wakiwa na lengo la kuwasaidia vijana wetu katika kupata elimu na kuisaidia Serikali katika kutoa huduma ya elimu kwa wananchi wake.

    (a) Je, Serikali inawasaidia vipi wazawa hawa wazalendo hasa ikizingatiwa uendeshaji wa vyuo hivi ni gharama kubwa.

    (b) Kwa nini Serikali haioni haja kwa wazawa hawa kuondolewa kodi (Tax holiday), ili waweze kuwekeza katika kutoa elimu iliyo bora kwa vijana wetu.

**Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:**

131. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:

    Pamoja na ongezeko la viwanja vya michezo vinavyojengwa katika maeneo ya Zanzibar, kumekuwa na malalamiko mengi kwa vijana juu ya matumizi ya viwanja hivyo katika kukuza sekta ya michezo hapa Zanzibar.

    (a) Je, ni sababu gani zinazofanya viwanja hivi kufungwa na kutofikiwa kwa malengo ya vijana kuvitumia.

    (b) Je, ni ipi khatma ya viwanja vya Maisara ambavyo vilikuwa vikitumiwa na wananchi na kwa sasa vimefungwa na

kuwekwa uzio.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

47. MHESHIMIWA MMANGA MOHAMMED HAMED (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Tumbe ni miongoni mwa sehemu hapa Zanzibar inayovuliwa sana dagaa, kiasi ambacho wafanyabiashara kutoka nchi za jirani wanakuja kulifuata dagaa hilo na kwenda kuliuza nchini mwao.

(a) Kwa nini Serikali haijengi viwanda vya kusarifu dagaa ili wananchi wa Tumbe hasa vijana wakapata ajira.

(b) Serikali inawahakikishia vipi wavuvi wa dagaa wa jimbo la Tumbe kupata soko la uhakika la kuuza dagaa kwa thamani yenye maslahi nao.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

10. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi.

Je, Serikali imeweka mikakati gani ya kuongeza umiliki wa ardhi kwa wanawake.

**Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi:**

87. MHESHIMIWA ALLEY MASOUD ALLEY (Jimbo la Mtambile) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Tunajua hivi karibuni Serikali ilizijenga barabara za Jaani kutokea Mauwani, Kengeja Likoni, Kengeja Kiimbini na Mahuduthi Kengeja, kupitia Sipwese shehia ya Mkungu. Pamoja na sababu nyengine, ni kuwa asilimia kubwa ya wananchi wa maeneo hayo ni wakulima.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwalipa fidia wananchi wote walioharibiwa vipando vyao vya kilimo, kwa ajili ya kupisha ujenzi wa barabara hizo.

92. MHESHIMIWA MOHAMMED ALI SALIM (Jimbo la Ziwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Kwa kuwa katika jimbo la Ziwani kumekuwa na tatizo kubwa la barabara za ndani za kufikia barabara kuu, hususan katika maeneo ya kijiji cha Pembeni kwenda katika Kituo cha Afya pamoja na skuli ya Ziwani. Na kwa kuwa jambo hilo huleta usumbufu mkubwa kwa wakulima, mama wajawazito pamoja na wanafunzi.

(a) Ni lini Serikali itazijenga barabara hizi, ili kuondoa usumbufu kwa wananchi wanaoishi katika maeneo hayo.

(b) Je, afya ya uzazi wa mama na watoto itapatikana vipi kutokana na uwepo wa barabara mbovu za ndani katika kijiji hicho.

<u>**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**</u>

245. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Mnamo mwaka 2011, Baraza la Mapinduzi lilitoa waraka maalum kuhusu kuimarishwa kilimo cha mpunga Zanzibar na kujitosheleza kwa mahitaji ya chakula na kuwekewa bajeti yake. Miaka mingi imepita hakujafanyika tathmini kutambua hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa agizo hilo la Serikali.

(a) Je, utekelezaji wa agizo hilo la Serikali la kuimarishwa kilimo cha mpunga ili Zanzibar ipunguze uagiziaji wa mchele, limefikia wapi.

(b) Na kama waraka huo haujatekelezwa au umeshindikana kutekelezwa au umefutwa, ni kwa sababu gani.

(c) Je, kuna tathmini gani imefanyika kutambua kiwango cha uzalishaji wa ndani wa mchele na kile kinachohitajika kuagiziwa nje.

**Wizara ya Afya:**

101. MHESHIMIWA MOHAMMED ALI SALIM (Jimbo la Ziwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kumekuwa na ongezeko kubwa la maradhi yasiyoambukiza katika maeneo mengi ya Unguja na Pemba. Maradhi hayo hupelekea kurundikana kwa wagonjwa wanaosubiri kupatiwa huduma za matibabu katika hospitali zetu za Wilaya na Vituo vya Afya.

Je, lini Serikali itawaboreshea matibabu wagonjwa hawa kwa kuanzisha *Mobile Clinic* katika miji na vijiji vyetu angalau mwezi mara moja, ili kuwapunguzia usumbufu walipa kodi hawa.

166. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kumekuwepo na maendeleo makubwa ya kiteknolojia katika matumizi ya vifaa vinavyotoa mionzi kwa ajili ya kupiga picha za kitabibu kwa binadamu katika hospitali na vituo mbalimbali vya kutolea huduma za afya nchini. Hata hivyo, matumizi ya teknolojia hizo yanahitaji usimamizi makini ili kuepusha madhara ya kiafya, kimazingira na kiusalama yanayoweza kusababishwa na matumizi yasiyo salama ya mionzi.

Je, ni upi mpango wa Serikali wa kuhakikisha kunakuwepo na matumizi salama ya vifaa vya mionzi kwa watendaji, wagonjwa, wananchi kwa ujumla na mazingira katika hospitali za umma na binafsi zinazotoa huduma hizo.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

72. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Imebainika hivi karibuni kuwa Wizara yako ilitoa ajira za mikataba kwa wafanyakazi kadhaa huko Pemba.

(a) Ni sababu zipi zilizoipelekea Wizara yako kutoa ajira hizi za mkataba.

(b) Ni wafanyakazi wangapi walipatiwa ajira hizi.

176. MHESHIMIWA SAID AZANA MSINGIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kwa muda mrefu sasa, shehia za Umbuji, Pagali na Bambi zina upungufu wa maji safi na salama kutokana na ukweli kuwa, maji yanayopatikana hayatoshi kwa matumizi ya wakaazi wa shehia hizo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa wananchi wa shehia hizo wanapata maji safi na salama yatakayowatosheleza katika shughuli zao.

## Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji:

175. MHESHIMIWA SAID AZANA MSINGIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Vijana, Ajira na Uwezeshaji:

Katika kuwainua vijana wetu ikiwa ni pamoja na vijana wa jimbo la Uzini, Serikali inawahamasisha vijana hao kujiajiri, kukuza vipaji vyao vya halali kwa njia mbalimbali zinazokubaliwa na sheria za nchi yetu.

Je, Serikali ina mipango ipi ya muda mrefu na muda mfupi ya kuhakikisha kuwa vijana wa jimbo la Uzini wanapata ajira na mitaji ya kuanzisha biashara zitakazokimu mahitaji ya maisha yao.

## Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:

108. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:

Pamoja na hatua kubwa ambazo dunia yetu inazipiga katika maendeleo ya kimitandao, kuna ongezeko kubwa la Wadukuzi (Hackers) wanaojipanga kuendeleza udukuzi kila uchao.

Kwa kuwa mapato yote ya Serikali kwa sasa yanapitia kwenye mifumo.  Je, Serikali imejipanga vipi kukabiliana na tatizo hili la kidunia.

III. **HOJA ZA SERIKALI:**

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

Mjadala wa Hotuba ya Uzinduzi wa Baraza la Kumi na Moja la Wawakilishi iliyotolewa tarehe 10 Novemba, 2025 na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

IV. **TAARIFA ZA SERIKALI:**

**Waziri wa Fedha na Mipango:**

Taarifa ya Muelekeo wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2026/2027.

**Zanzibar,**
**17 Februari, 2026.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA LA WAWAKILISHI, ZANZIBAR**